# Wakulima, wafugaji kuanzishiwa miradi ili kukomesha migogoro

**Na MWANDISHI WETU**

SERIKALI imesema katika kuboresha na kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini ukiwemo Mkoa wa Morogoro, inasisitiza uwepo wa miradi ambayo itakuwa na manufaa makubwa kwa makundi yote mawili.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Profesa Elisante Ole Gabriel, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita, Wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro, alipotembelea ujenzi wa mradi wa kiwanda cha nyama katika Ranchi ya Nguru Hills na kubainisha mradi huo unaotarajia kukamilika Aprili, mwakani, utakuwa na manufaa makubwa kwa wafugaji na wakazi wa mkoa huo.

"Tumekuja kuangalia shughuli zinazoendelea kutokana na kikao ambacho tulikuwa nacho katika ofisi ya katibu tawala wa mkoa na mkuu wa mkoa wa Morogoro, kwa lengo la kuboresha shughuli za mifugo kwenye mkoa huo na kuondoa changamoto

> **Mradi huu una jambo mahsusi kuliko mingine, maji haya ya mabwawa yatatumika kwa ajili ya umwagiliaji huu ni moja kati ya miradi ambayo wafugaji na wakulima watanufaika ili wote waone huu mradi ni wa kwao kwa ajili ya uchumi wetu.**
>
> Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel

za migogoro ya wafugaji. Uongozi wa mkoa waliniambia juu ya mradi huu, ambao utakuwa na msaada mkubwa sana kwa wakulima na wafugaji wa mkoa wa Morogoro na nchi kwa ujumla," alisema.

Profesa Gabriel, alibainisha kuwa mradi huo wa kipekee, baada ya kiwanda hicho kukamilika, utakuwa na uwezo wa kuchinja mbuzi zaidi ya 200 na ng'ombe zaidi ya 1,000 kwa siku.

Pia, alisema kumejengwa mabwawa makubwa yatakayotumika kukusanya maji yanayotoka kwenye machinjio, kisha kutibiwa kabla ya kutumika tena kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

"Mradi huu una jambo mahsusi kuliko mingine, maji haya ya mabwawa yatatumika kwa ajili ya umwagiliaji. Huu ni moja kati ya miradi ambayo wafugaji na wakulima watanufaika ili wote waone huu mradi ni wa kwao kwa ajili ya uchumi wetu," alisema

Aidha, alisema mradi huo wenye thamani ya zaidi ya sh. bilioni 25, ambao unashirikisha wabia mbalimbali, ukiwemo Mfuko wa Pesheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ni azma ya serikali katika kuzidi kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwenye sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya mifugo.

Aliwataka wafugaji kuboresha mifugo yao kwa kufuga ng'ombe bora wa kisasa na kupitia miradi ya kunenepesha mifugo ili waweze kuuza mifugo yenye ubora katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo hapa nchini ili sekta izidi kukua na kuchangia pato la taifa kupitia uchumi wa viwanda.

Pia, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha Tanzania inakuwa na mifugo mingi na bora kwa kuhakikisha mifugo inaogeshwa ili kujikinga dhidi ya magonjwa na kuwataka wakurugenzi wa halmashauri kote nchini, kuhakikisha maeneo yao yana majosho ya kutosha kwa ajili ya kuogeshea mifugo na kuwataka wayafanyie ukarabati majosho ambayo hayafanyi kazi.

"Tufuge kisasa. Namibia, Botswana wana ng'ombe wachache, lakini wanauza kwa wingi nyama nje ya nchi, ndiyo maana tunaimarisha afya za mifugo, ndiyo maana nchi nzima tunashughulika na masuala ya uogeshaji. Niwatake wakurugenzi wa halmashauri, wahakikishe kwenye maeneo yao, kuna majosho ya kutosha na niwatake yale ambayo hayafanyi kazi vizuri yaboreshwe," alisema.



Uhuru uk8, Tarehe 30/11/2020

Scanned with CamScanner

nye benki yao katika mahesabu ilikuwa Sh. 76,880,300 wakati uhalali ni Sh. 47,880,300 kinyume cha kifungu cha 317 (b) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 marejeo ya mwaka 2019.

taka yao mawili, lakini waliyakana.

Washtakiwa wako nje kwa dhamana ya wadhamini wawili wawili, ambao walitoa barua za utambulisho kutoka kwa ofisa

hiyo hadi Desemba 10, mwaka huu kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Masambu

ripoti yao ilionyesha kwamba salio lililokuwamo kwenye benki yao katika mahesabu ilikuwa ni Sh. 76,880,300 wakati uhalali ni Sh. 47,880,300 kinyume cha sheria.

# Serikali yasisitiza miradi kutatua migogoro ya wakulima, wafugaji

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema katika kuboresha na kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo Mkoa wa Morogoro, imeendelea kusisitiza uwapo wa miradi ambayo itakuwa na manufaa makubwa kwa makundi hayo mawili.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, aliyasema hayo alipotembelea ujenzi wa mradi wa kiwanda cha nyama katika Ranchi ya Nguru Hills mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki.

Alisema mradi huo unaotarajia kukamilika Aprili mwaka 2021, utakuwa na manufaa makubwa kwa wafugaji na wakazi wa mkoa wa Morogoro.

Prof. Gabriel alisema kuwa mradi huo wa kipekee, baada ya kiwanda hicho kukamilika, kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe zaidi ya 200 na mbuzi 1,000 kwa siku.

Alisema tayari kumejengwa mabwawa makubwa ambayo yatakuwa yanakusanya maji yanayotoka kwenye machinjio na kuyatibu kabla ya kutumika tena kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

Prof. Gabriel alisema mradi huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 25, ambao unashirikisha wabia mbalimbali ukiwamo Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ni azma ya serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji hapa nchini.

Alisema kupitia mradi huo, wafugaji wataboresha mifugo yao kwa kufuga ng'ombe bora wa kisasa na kuinenepesha ili iwe yenye ubora.

Pia alisema utasaidia katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo hapa nchini kwa lengo la kukuza pato la nchi kupitia uchumi wa viwanda.

Prof. Gabriel alilitaka dawati la sekta binafsi lililo chini ya wizara hiyo, pamoja na idara ya uzalishaji na masoko kwa kushirikiana na PSSSF kukutana haraka ili kujadili changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika mradi wa kiwanda cha nyama Nguru Hills ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Hassan Chama, alimhakikishia Katibu Mkuu huyo kuwa kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wafugaji na kuwaondolea changamoto ya kuuza mifugo yao kupitia minada ambayo wamekuwa wakikutana na madalali ambao wanafanya bei za mifugo kuwa chini.

Mradi wa kiwanda cha nyama katika Ranchi ya Nguru Hills unaotarajia kukamilika Aprili mwakani, unategemewa kutoa ajira kwa wafanyakazi 120 hadi 200 kulingana na uzalishaji.

Nipashe uk 7, Tarehe 30/11/2020

Scanned with CamScanner

# Sekta ya uvuvi 'inakoelekezwa' kuineemesha Tanzania kiuchumi

*Na Jonas Kamaleki*

UVUVI ni 'chimbo jingine lenye rasilimali zenye thamani' kama ilivyo madini ya Tanzanite, dhahabu na almasi, kutokana na kwamba unaweza kukuza haraka uchumi wa Tanzania endapo utasimamiwa na kudhibitiwa kwa umakini.

Tanzania imebarikiwa kuwa na bahari, maziwa, mito na mabwawa, ambavyo vikitumiwa vizuri kwa shughuli za uvuvi, vitainua uchumi wa nchi na kupunguza umaskini wa kipato cha mtu mmoja na taifa kwa ujumla.

Akihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Magufuli, siku hiyo pia akizindua bunge hilo, alisema kuhusu sekta ya uvuvi:

"Nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yanayofaa kwa shughuli za uvuvi, ikiwemo Ukanda wa Pwani, maziwa, mito na mabwawa.

"Hali hii inafanya sekta hii kuwa na nafasi ya kutoa mchango mkubwa kwenye kukuza pato la taifa. Na pia kupambana na umasikini na tatizo la ajira.

"Hata hivyo, kwa sasa, mchango wake bado ni mdogo.

"Hivyo basi, kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuikuza sekta hii, ikiwemo kuimarisha shughuli za uvuvi kwenye baharikuu, ambako tumekuwa tukipoteza mapato mengi."

Kuhusu kuthamini na kuamini kuwa uvuvi utakuza uchumi wa nchi kwa kasi, Rais wa Zanzibar, Dkt Hussein Ali Mwinyi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ameunda Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi. ambayo anaamini kwamba itakuwa mkombozi wa uchumi wa nchi hiyo.

***Uchumi wa Bluu*** unajumuisha utalii, uvuvi, mafuta na gesi.

Dkt Mwinyi amesema kuwa bahari haijatumika kiasi ambacho inapaswa inufaishe nchi, hasa kwenye uvuvi.

Amesema kuwa Zanzibar inabidi ijipange kufanya uvuvi wenye tija, hasa kwenye baharikuu, ili uchangie kwa kiwango kikubwa kukuza pato la taifa, na hivyo kuboresha maisha ya Wazanzibar.

Ujenzi wa bandari za uvuvi na viwanda vinavyotumia malighafi zipatikanazo baharini, ikiwemo samaki, vitasaidia kukuza uchumi wa Zanzibar, ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtazamo wa Dkt Mwinyi unafanana na wa Dkt Magufuli kuhusu kukuza uchumi kwa kutumia uvuvi.

Akisisitiza kuhusu ukuzaji uchumi kwa kutegemea uvuvi, Rais Magufuli alisema:

"Kwa mujibu wa ripoti ya kamati ya bunge kuhusu shughuli za uvuvi wa baharikuu ya mwaka 2018, shughuli za uvuvi kwenye baharikuu zinaweza kuingizia serikali mapato ya moja kwa moja ya takriban shilingi bilioni 352.1 kwa mwaka, endapo mifumo ya usimamizi na udhibiti ingekuwa imara, na samaki wangechakatwa hapa nchini.



*"Kwa mujibu wa ripoti ya kamati ya bunge kuhusu shughuli za uvuvi wa baharikuu ya mwaka 2018, shughuli za uvuvi kwenye baharikuu zinaweza kuingizia serikali mapato ya moja kwa moja ya takriban shilingi bilioni 352.1 kwa mwaka, endapo mifumo ya usimamizi na udhibiti ingekuwa imara, na samaki wangechakatwa hapa nchini ....*



**Samaki wa Sangara ambao hupatikana Ziwa Victoria ni moja ya rasilimali muhimu wa chakula na vipato.** (Picha ya mtandaoni)

"Hata hivyo, mapato yaliyokuwa yamekusanywa kwa kipindi cha miaka tisa (2009 hadi 2017) yalikuwa shilingi bilioni 29.79, sawa na shilingi bilioni 3.3 kwa mwaka. Kiwango hiki cha mapato hakikubaliki."

Rais Magufuli alibainisha kuwa, serikali inataka katika miaka mitano ijayo, isimamie vizuri shughuli za uvuvi wa baharikuu, ili taifa linufaike na rasilimali zake.

Kuhusisha sekta binafsi, alisema kuwa, bahati nzuri, tayari, mwaka huu (2020) imetungwa sheria mpya ya kusimamia na kuendeleza uvuvi wa baharikuu.

"Aidha, tumepanga kununua meli 8 za uvuvi kwa kushirikiana na shirika la IFAD (4 upande wa Zanzibar na 4 upande wa Tanzania Bara), ili zishiriki katika uvuvi wa baharikuu.

"Kama mnavyofahamu, suala la uvuvi wa baharikuu ni la Muungano. Tunakusudia pia kujenga bandari kubwa ya uvuvi itakayotoa ajira zipatazo 30,000.

"Na tutaendelea kuhamasisha sektabinafsi kujenga viwanda vya kuchakata samaki," Rais Magufuli alisema.

Sambamba na kusimamia baharikuu, serikali pia imejipanga kuimarisha shughuli za uvuvi kwenye maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), pamoja na mito mikubwa kama vile Ruvu, Rufiji, Malagarasi, Kagera na Kilombero.

Wavuvi wadogo watahamasishwa kujiunga kwenye vikundi, ili waweze kupatiwa mitaji, ujuzi, vifaa, zana za uvuvi na haliadhalika.

Serikali imejipanga kupitia upya tozo za maeneo mbalimbali, ili kuwapunguzia wavuvi kero na kuvutia uwekezaji.

Uhamasishaji wa watubinafsi kujenga mabwawa na kufuga kisasa kwa kutumia vizimba pia utafanyika.

Sekta ya uvuvi ni lazima itoe mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi.

Nchi ndogo ya Norway ambayo haina maziwa wala mito kama Tanzania, sekta ya uvuvi ni ya tatu kwa bidhaa za nchi hiyo zinazouzwa nje, baada ya mafuta/gesi na metali.

Hivyo sekta hiyo hutoa mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi hiyo.

Tanzania haina budi kuwe[illegible]za zaidi na kusimamia 'chimbo jingine lenye rasilimali zenye thamani' hilo, kwa ajili ya uchumi endelevu na wenye tija.

Scanned with CamScanner